

Simu: 0754 895 391,
Barua Pepe: milambo@gmail.com,
MWANZA.
24/11/2022.

Mkurugenzi Mkuu,
Shirika la Reli Tanzania,
S.L.P 76956,
DAR ES SALAAM.

Ndugu,

Yah: OMBI LA KAZI YA FUNDI UMEME

Mimi ni mwanamume mwenye umri wa miaka 30. Ninaomba Kazi ya Fundi Umeme kama ilivyotangazwa na Shirika la Reli Tanzania siku ya tarehe 28/11/2022 katika Tovuti, mitandao ya Kijamii na mbao za matangazo.

Nina Cheti cha Fundi Umeme nilichotunukiwa kutoka VETA mwaka 2020. Pia, nina uzoefu wa kufanya kazi na nimefanya kazi na Taasisi Ya 21st Century Holding LTD.

Kutokana na elimu yangu, uwezo wa kufanya kazi nilionao, uzoefu, pamoja na kuwa na sifa zinazotakiwa, ninaamini kuwa ninastahili kupata kazi hii. Endapo nitapata kazi hii ya Fundi Umeme, nitafanya kazi kwa bidii kama ilivyoelekezwa. Baadhi ya majukumu yangu ni: kutengeneza mifumo ya umeme, kuhakikisha vifaa vya umeme vinafanya kazi na kufuata maelekezo nitakayopangiwa.

Nipo tayari kwa usaili siku yoyote nitakayohitajika. Vilevile, ninatarajia majibu mazuri kutoka kwako na nimeambatanisha nakala ya vyeti vyangu kwa uthibitisho zaidi.

Wako mtiifu,

Japheth Michael